



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI



TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

**UCHAGUZI MDOGO WA MADIWANI KATIKA KATA
MBILI ZA TANZANIA BARA**

Kwa mujibu wa Kifungu cha 13 (1) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Waziri mwenye dhamana ya Serikali za Mitaa aliitaarifu Tume uwepo wa nafasi wazi za Madiwani katika Kata ya Kelamfua iliyoko katika Halmashauri ya Wilaya ya Rombo na Kata ya Kitaya iliyoko katika Halmashauri ya Wilaya ya Nanyamba. Nafasi zote mbili za Udiwani zimetokana na kujiuzulu kwa madiwani waliokuwa wamechaguliwa awali.

Kata zilizowazi:

| Na | MKOA | HALMASHAURI | KATA |
|----|-------------|-----------------------------------|----------|
| 1. | Kilimanjaro | Halmashauri ya Wilaya ya Rombo | Kelamfua |
| 2. | Mtwara | Halmashauri ya Wilaya ya Nanyamba | Kitaya |

Kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 13(3) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Tume inatoa taarifa kwa umma kuhusu uwepo wa Uchaguzi mdogo wa Madiwani katika Kata hizo utakaofanyika kwa kufuata ratiba ifuatavyo:


Ratiba ya Uchaguzi mdogo huo ni kama ifuatavyo:

| NA. | TUKIO | TAREHE |
|-----|----------------------------|-------------------------------------|
| 1. | Uteuzi wa Wagombea Udiwani | 16 Julai, 2018 |
| 2. | Kampeni za Uchaguzi Mdogo | 17 Julai, 2018 hadi 11 Agosti, 2018 |
| 3. | Siku ya Kupiga kura | 12 Agosti, 2018 |

Tume ya Taifa ya Uchaguzi inavialika Vyama vya Siasa, Wadau wote wa Uchaguzi na Wananchi kwa ujumla kushiriki Uchaguzi huo kwa kuzingatia ratiba, sheria, kanuni, maadili ya Uchaguzi, miongozo na maelekezo ya Tume wakati wa kipindi chote cha Uchaguzi mdogo.

Aidha, Kwa mujibu wa kifungu cha 41(2) cha Sheria ya Uchaguzi ya Serikali za Mitaa, Tume ya Taifa ya Uchaguzi inaviarifu Vyama vya Siasa na Wananchi wote kuwa Uteuzi wa Wagombea uliokuwa umepangwa kufanyika siku ya Jumamosi tarehe 14 Julai, 2018 kwa ajili ya Uchaguzi Mdogo katika Kata za Tindabuligi na Kisesa kwenye Halmashauri ya Wilaya ya Meatu, Kata ya Katumba iliyopo Halmashauri ya Wilaya ya Nsimbo na Kata ya Mlimba katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero umeahirishwa. Tume itatangaza hapo baadae tarehe nyingine za uteuzi na uchaguzi katika Kata hizo.

Imetolewa leo tarehe 10 Julai, 2018.


Jaji (R) Semistocles S. Kaijage
MWENYEKITI
TUME YA TAIFA YA UCHAGUZI